**Muhimu:**

i. Fomu iliyoambatanishwa na barua hii ni ya kupima afya ya mwanao, baada ya kupimwa na daktari aliyethibitishwa, ijazwe na kupigwa muhuri wa daktari husika na kuletwa chuoni siku ya kuripoti.
ii. Chuo hakitahusika na kuwasafirisha wanachuo hivyo kila mzazi/mlezi anao wajibu wa kumsafirisha mwanachuo kuja chuoni na kurudi nyumbani.

Fuata maelekezo yote kwa usahihi ili kuepuka usumbufu.

**SHERIA NA KANUNI ZA CHUO CHA**

**CHRIST AMBASSADORS.**

**MWAKA 2016/2017**

SOMA KWA MAKINI.

Ni wajibu wa kila mwanachuo kufahamu na kutii amri na kanuni za Chuo kwa makini.Mwanachuo atakayevunja sheria ama kwenda kinyume na kanuni za chuo aidha ataadhibiwa au atarudishwa nyumbani kwa muda Mwanachuo asiyeweza kubadili tabia yake mbovu atafukuzwa toka chuoni.

SHERIA NA KANUNI ZA CHUO

1. Ni lazima kila mwanachuo kuhudhuria vipindi vyote na kufanya mazoezi, majaribio na mitihani atakayopewa na wakufunzi au watahini wengine (NACTE) nk.

2. Ni lazima kila mwanachuo kuhudhuria ibada zinazoendeshwa kwa mujibu wa imani ya kikristo.

3. Ni lazima kila mwanachuo awe amevaa sare ya chuo wakati wa vipindi darasani na avae sare ya chuo anapokuwa nje ya chuo.

4. Ni lazima kila mwanachuo kuheshimu wakufunzi, wafanyakazi wengine wa Chuo, wazazi na viongozi wote wa kanisa na serikali ya wanafunzi.

5. Wanachuo hawaruhusiwi kuvaa kofia, yebo yebo, kandambili, au viatu vya wazi wanapokuwa darasani au ibadani.

6. Wasichana hawaruhusiwi kuvaa bangili, shanga za shingoni au kujipamba kwa kupaka rangi au wanja midomoni, nk.

7. Mwanachuo haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila kibali cha Mkuu wa shule au Matron. Ruhusa zote za kwenda mjini au nyumbani hutolewa na Mkuu wa Chuo pekee.

